UKAMILIFU

. . .Na kuwa hapa kuabudu pamoja nanyi. Na sasa kabla tu ya Ujumbe, ninaye rafiki yangu mwema hapa jukwaani usiku wa leo, Daktari Lee Vayle, kutoka kanisa la Kwanza la Baptisti huko Lima, Ohio, ambaye alikuwa mmoja wa wafadhili wangu kwenye mkutano wa Lima. Nilimuuliza, nikishuka kuja usiku wa leo, kama hatasema tu neno kwa kusanyiko, labda kuhusiana na mkutano wa Lima, kwa dakika moja ama mbili zifuatazo. Nami nina furaha kuwa, nina furaha kuwajulisha usiku wa leo, Daktari Lee Vayle, Mbaptisti mwingine aliye na Roho Mtakatifu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

2 Amina. Mungu akubariki, Ndugu Vayle, pia.

3 Hiyo ilikuwa motomoto sana kwa mchungaji Mbaptisti, sivyo? Vema, tuna furaha sana kuwa na Ndugu Vayle pamoja nasi. Na bila shaka milango iko wazi kwake kurudi na kututembelea wakati wowote awezao. Na sasa usiku wa leo . . .

Kesho usiku ndio—*Kuzikwa* kwa Bwana Yesu.

4 Jumapili asubuhi ni ibada ya mapambazuko ya thenashara. Nami ninaamini ndugu ametangaza sehemu zaidi ya ibada.

Sasa hebu na tuombe kwa dakika moja.

5 Bwana mbarikiwa, Neno Lako ni Kweli, nasi tunashukuru kwa ajili ya watu wanaolishika, bila woga, wanapolitoa kwa watu. Na tunapoifungua Biblia usiku wa leo, ama kuzifungua kurasa Zake, Roho Mtakatifu mbarikiwa na aje na kutufungulia Neno la ufahamu. Kupitia kwa Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

6 Usiku huu mkuu tunaosherehekea, wa kusulubiwa kwa Bwana wetu mbarikiwa, ningependa kusoma usiku wa leo kutoka katika midomo Yake Mwenyewe ya thamani, Maneno ambayo Yeye ameandika katika Kitabu Chake. Katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 4, sisi. . .na kifungu cha 47 na 48, tunasoma hivi:

> *Tena mkiwaamkua ndugu zenu tu, je, mnafanya nini zaidi ya wengine? hata watoza ushuru hawafanyi hivyo?*
>
> Lakini *kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*

7 Basi usiku wa leo tulitangaza ya kwamba tutazungumza juu ya somo la *Ukamilifu.* Sasa sisi. . .Hilo linaonekana kama fungu la maneno ya kigeni sana kuchukua kwa usiku wa kusulubiwa kwa Bwana wetu. Lakini leo, pengine, mmekuwa mkisikiliza redio, na kusikia jumbe mbalimbali na wajumbe, jinsi walivyoiwasilisha siku hiyo ya kutisha wakati Bwana wetu alipokufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Kwa hivyo nimechagua, usiku wa leo, kuzunguka kwa njia tofauti,

kulifikia, kwa hivyo itakuwa tofauti kidogo na inaweza kuwaburudisha kidogo. Roho Mtakatifu mbarikiwa na alivuvie Neno sasa tunapofanya juhudi kulileta.

8 Mungu anahitaji ukamilifu. Tunataka kukumbuka hilo, ya kwamba hakuna kitu nusu nusu tu kinachoweza kwenda katika Uwepo wa Mungu. Hakina budi kuwa kikamilifu, ibada yetu, kila kitu.

9 Sasa, katika bustani ya Edeni, Mungu alikuwa na Adamu na Hawa katika hiyo bustani. Nao wakafanya dhambi na kuzivunja sheria za Mungu, kwa kutenda dhambi, uasi. Basi uasi unapokuja, kutotii ni kuiasi sheria. Na sheria ya Mungu, Yeye akiwa ni mtakatifu, mtakatifu asiyeghoshiwa, kwa hiyo hakuna doa la unajisi linaloweza kusimama Mbele Zake. Kwa hiyo, ikiwa dhambi ilikuja ulimwenguni kwa uasi, basi dhambi lazima ishughulikiwe kabla mwenye dhambi hajapata kusimama Mbele za Mungu.

10 Sasa, kama hakuna sheria, basi hakuna haki. Lakini sheria ilihitaji, au, haki inahitaji sheria. Nayo sheria, wakati i—inapotumiwa, inaonyesha haki.

11 Sasa, kwa sheria, hakuna mwenye mwili anayeokolewa. Sasa, sheria haiwezi kutuokoa. Sheria ilikuwa tu ni kitu kilichotufunga gerezani, lakini haina nguvu za ukombozi. Sheria ilituonyesha tu kwamba tulikuwa wenye dhambi, na ikatuhukumu. Hivyo ndivyo sheria inavyopaswa kufanya. Ni kuleta hukumu, au kukuonyesha kosa lako lilipo. Kwa hiyo sheria, yenyewe, haingeweza kuokoa. Ingeweza tu kushtaki.

12 Naye Mungu, akiwa mtakatifu na mwenye haki, ilimbidi awe na mashtaka. Ilimbidi kumshtaki mwenye dhambi kwa sababu alikuwa amevuka mipaka ya neema, naye akawa raia mvunja sheria. Ndipo, hana budi kushughulikiwa.

13 Na kila sheria ina adhabu, kwa maana, adhabu ya kuasi sheria ya Mungu ni mauti. Nayo ilibidi kuionyesha kifo jamii ya binadamu. Nayo jamii yote ya binadamu iko chini ya adhabu ya sheria hii.

14 Sasa, Adamu na Hawa walipokuwa wametenda dhambi, hapakuwapo na njia, hakuna dawa nyingine ambapo wangeweza kusimama Uweponi mwa Mungu tena, isipokuwa dhambi hii ishughulikiwe. Wala hakuna mtu anayeweza kutenda dhambi ya aina yoyote, haijalishi ni ndogo au kubwa jinsi gani, dhambi hiyo moja haina budi kushughulikiwa kabla yule aliyeitenda hajapata kusimama Uweponi mwa Mungu Mtakatifu.

15 Hivyo, basi, Adamu na Hawa walipokuwa wamefanya dhambi na kuvunja sheria, walipasiwa kifo. Nayo sheria ilibidi kutekelezwa, kwa hiyo iliweka jamii yote ya binadamu chini ya adhabu ya kifo. Sasa kama tunaweza tu kutulia kwa muda mchache sasa, katika mawazo yetu, na kuitazama picha hii kuu, na kukumbuka kwamba kila mtu hapa amejumuishwa katika

hili. Kila mwanamume na mwanamke, mtoto, amejumuishwa katika adhabu ya kifo, kwa ule uasi wa kiongozi wa jamii ya binadamu, Adamu; kwa uasi wake, kila mmoja wetu akawa mwathiriwa wa dhambi.

16 Nayo dhambi haina budi kushughulikiwa. Na kwa hiyo, Mungu, katika ukuu Wake usio na kikomo na upendo Wake mkuu. . . Sheria ilikuwa ya kumtenga mwenye dhambi na Muumba wake; kisha akaangamizwa, na kuangamizwa kabisa, kamwe hakungekuwa na njia kwake kurudi isipokuwa dhambi hiyo ishughulikiwe. Basi ingekuwa ni rahisi sana kuamini katika maangamizi kamili ya mwenye dhambi mwishoni, kwa maana ametengwa kabisa, milele na Uwepo wa Mungu.

17 Sasa angalieni dhambi hii. Na jinsi Mungu, akiwa mwenye haki, wala asingeweza kufanya lolote lingine ila kuwa mwenye haki, kwa maana Yeye ndiye chanzo cha haki yote, basi kusingekuwa na kitu kingine chochote cha kufanya ila kuweka adhabu ya uasi huu. Nayo hiyo adhabu ilikuwa ni mauti, kwa kuwa Yeye alisema, "Siku utakapokula, siku hiyo hakika utakufa." Sasa, ni picha nyeusi tuliyo nayo hapa.

18 Lakini basi kama tungerudi nyuma kidogo tu, tupate kujua sifa zanyewe za Mungu, Biblia inatwambia dhahiri ya kwamba "Mungu ni upendo." Lakini hata hivyo, akiwa ni upendo, hana budi kuwa mwenye haki. Kwa hiyo, upendo haumaanishi kitu tu ambacho kinaweza kudekezwa na kuchezewa. Upendo ni haki ya Mungu.

19 Sasa, Mungu alipoona ya kwamba watoto Wake walikuwa wameiasi sheria Yake, na ya kwamba hawana budi kufa kile kifo, basi upendo mkuu uliingia upate kufanya njia. Kwa maana, Mungu aliona ya kwamba watoto hawa kweli wataangamia kabisa, kabisa watoke Uweponi Mwake. Hakukuwako na kitu kingine cha kufanywa, kwa kuwa walikuwa wameivunja sheria Yake, na adhabu ya sheria Yake ilikuwa ni mauti.

20 Ndipo upendo wa Mungu ukawaendea raia Wake. Basi upendo wa Kiungu unapoonyeshwa, neema kuu hutoa madhumuni ya upendo. Naye Mungu, kwa kujua tangu zamani, alipoipenda sana jamii Yake; hata hivyo, pamoja na adhabu, Yeye alisababisha kifo cha kibadala kutokea katika bustani ya Edeni. Hiyo ilikuwa, Yeye aliweka kibadala cha kiumbe asiye na hatia, maskini mwana-kondoo asiyejua dhambi, naye akawa kibadala, kutenda kazi na kufa badala ya huyo mwenye dhambi aliye na hatia. Naye alikuwa ni mwana-kondoo, aliyechinjwa, kuushikilia uhai wa raia Wake.

21 Kote katika Agano la Kale walitoa damu ya wana-kondoo na mbuzi, kondoo, mafahali na ndama, kifo kibadala. Lakini, yote katika uchumi mkuu wa Mungu, alikiwazia niani Mwake kuja kwa kile Kitu halisi, ambacho kingekuwa. . . Hayo yalikuwa ni vivuli vya kile Kitu halisi kijacho. Nacho kile Kitu halisi

kilichokuwa kinakuja, kilikuwa ni Mwanawe wa pekee. Wanakondoo wote waliokufa walikuwa ni kivuli tu. Nacho kivuli ni upande hasi tu wa kitu fulani. Nao walinena tu juu ya kuja kwa Kalvari.

22 Sasa kwa ajili ya picha ya jambo hili, hebu na tufungue Biblia zetu, kwenye Kitabu cha Waebrania, na tuchukue hapa yale Paulo, yule mtume mashuhuri akizungumza, akijaribu kutenganisha mambo haya kwa ajili yetu. Katika mlango wa 10 wa Kitabu cha Waebrania, tunasoma hivi.

23 Nami nalipenda tu Neno! Neno ni Kweli. Nami napenda kulisoma mbele ya kusanyiko langu, kwa sababu ninajua ya kwamba katika hukumu nitasimama pamoja nao. Nami sina budi kutoa hesabu. Kwa hiyo nikilileta kutoka kwenye Neno, basi sitakuwa na hatia; kwa sababu ni Neno, naye Mungu anawajibikia Neno Lake.

24 Tunaona mengi sana siku hizi, ya wainjilisti na kadhalika, wakijenga watu binafsi. Loo, ni jambo la aibu! Nasi tunaona, katika kuingia makanisani, tunaingia kanisani nawe unamkuta mchungaji fulani, ana kitendo chake kidogo cha kipekee, maskini mhemuko fulani. Usipoangalia, kusanyiko lote litachukua roho hiyo. Ikiwa ni mwenye jazba kidogo tu, au hutikisa kichwa chake, au maskini jambo fulani la kipekee, vema, kanisa zima litachukua hilo. Nasi, siku hizi, katika makanisa yetu ya kisasa, tumefikia ambapo kuna misisimko na mambo madogo kama hayo. Na imeleta mchafuko mkubwa sana! Lakini, loo, ndugu zangu wapendwa, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo tunapaswa kuwa kwenye Neno, ni leo hii!

25 Unaona, ningechukia kusimama kwenye hukumu na kujua ya kwamba nilikuwa na maskini kitu kigeugeu cha maskini ufunuo wa kipekee, na kuwapoteza watu. Sitaki wapate roho yangu juu ya matendo yangu, bali ninawataka wawe na Roho wa Mungu kwa Neno la Mungu, linalozaa Kweli.

26 Kwa hiyo katika tukio hili kuu usiku wa leo, ningependa kusoma kutoka katika Neno la Milele la Mungu. Sasa tunatambua kwamba sheria ilidumu miaka mingi, lakini sheria isingeweza kamwe kuiondoa dhambi. Kama nilivyosema hapo awali, ilikuwa ni nyumba tu ya magereza. Ilikuwa ni mpelelezi mkuu aliyekwambia ulichofanya, lakini hakuwa na suluhisho la kukukomboa. Ilikuweka kwenye duka la rehani, lakini hapakuwapo na Mkombozi wa kukutoa humo, nayo. Inakufunga tu gerezani, kukujulisha kuwa ulikuwa mwenye dhambi. Lakini sasa angalia katika Waebrania, mlango wa 10, tunaposoma.

Kwa kuwa torati ni kivuli tu cha mambo mema yajayo, wala si sura . . .

27 Kumbuka, ilikuwa ni kivuli cha sura inayokuja. Kivuli hutambulisha tu kwamba kuna sura inayofanya kivuli. "Kivuli

cha mambo yajayo, wala si sura yenyewe." Angalia, "ya mambo . . ."

> *. . .sura yenyewe ya mambo hayo, haiwezi kwa dhabihu zile walizozitoa. . . haiwezi wakati wowote kumkamilisha* akaribiaye.

28 Sasa, Mungu, hapo mwanzo, alihitaji ukamilifu. Yesu, alipokuja duniani, alisema, "Iweni wakamilifu, kama vile Mungu Mbinguni alivyo mkamilifu." Nayo torati, ikiwa ni kivuli cha mambo yajayo, haingeweza kamwe kumkamilisha mwabuduo. Mnaipata hiyo picha? Sasa hebu tuliendee tena ili mhakikishe hamtalikosa. Mungu anahitaji utakatifu mkamilifu. Hakuna awezaye kusimama katika mfano Wake, akiwa na chembe moja ndogo ya dhambi. Yesu alishuhudia vivyo hivyo, na kusema, "Iweni wakamilifu, kama tu vile Mungu Mbinguni alivyo mkamilifu."

29 Nayo Biblia ilisema kwamba, "Sheria isingeweza kamwe, pamoja na dhabihu zake, kumkamilisha akaribiaye." Basi, sheria isingeweza kukamilisha chochote. Ilikuwa ni kielekezi tu. Dhabihu hizi, zilizotolewa kila mwaka, kamwe hazingeweza kumkamilisha mwabuduo. Hivyo basi, hakuna mtu chini ya sheria, au akiishika sheria, au chini ya vile vivuli, angeweza kuwa mkamilifu.

> Kwa kuwa (kifungu cha 2) *basi hazingekoma kutolewa?. . .*

30 Kama kuna jambo lolote ninaloweza kufanya ili kujifanya mkamilifu Mbele za Mungu, basi Kristo hakupaswa kufa kwa ajili yangu. Kama kuna jambo moja unaloweza kufanya, ambalo lingestahili chochote Mbele za Mungu, basi Kristo alikufa bure. Hakuna kushika sheria, hakuna mawazo yako ya kisheria, hakuna utakatifu wako mwenyewe, hakuna mambo ambayo ungeweza kuacha kufanya, kuacha uwongo, kuacha wizi, kuacha kuvuta sigara, kuacha kwenda kwenye sinema, bado umepotea. Hakuna kiwezacho! Kujiunga na makanisa, desturi, sherehe, mabatizo, maagizo ya kanisa, kusoma kanuni za imani, kukariri sala, mambo hayo yote ni bure. Umepotea! Hakuna hata jambo moja unaloweza kujifanyia mwenyewe, kwa kuwa wewe ni mwenye dhambi chini ya hukumu. Wala hakuna njia yoyote ndani yako, wala kanuni yoyote ya imani, wala chochote unachoweza kufanya ama kuwazia, wewe mwenyewe, ambacho kinaweza kustahili jambo moja Mbele za Mungu, kwa maana kwanza kabisa wewe ni mwenye dhambi.

31 Nayo Biblia inatangaza, ya kwamba sisi sote tulizaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo. Wala Mungu asingeweza kumchukua mtu mmoja afe kwa ajili ya mwingine, kwa maana mmoja ana hatia tu kama huyo mwingine. Mbele za Mungu, askofu mkuu aliyezaliwa katika ulimwengu huu alikuwa na hatia kama

kahaba duni sana wa baa mjini. Mmoja hawezi kumfanyia mwingine upatanisho.

32 Kwa hiyo, Yeye alichukua uhai usio na hatia wa mnyama, maskini mwana-kondoo. Na chini ya Agano la Kale, torati ilikuwa, mtu alipotenda dhambi, alimleta mwana-kondoo madhabahuni. Tuseme kama alivunja amri yoyote, alimleta mwana-kondoo akamlaza madhabahuni, akaweka mikono yake juu ya huyo mwana-kondoo naye akaungama dhambi zake, ya kwamba alikuwa amekosea na alijua ya kwamba alikuwa na hatia. Ya . . . na ilikuwa . . . Sheria ilihitaji mauti. Naye akamleta mwana-kondoo badala yake. Ndipo wakati yeye . . . Koo la maskini mnyama huyo lilikatwa, naye akaanza kurusha maskini mateke yake, na kulia. Kama umewahi kuona mwana-kondoo akichinjwa, ni kilio cha kuhuzunisha jinsi gani! Maskini jamaa huyo akijaribu kulia, huku maskini mshipa wake wa shingo umekatwa. Basi anarusha mateke na kutetemeka, na akijinyosha, kisha anatetemeka tena na kulia, na damu inabubujika, inaosha maskini sufu yake pamoja na mikono ya mwabuduo.

33 Basi mwabudu anapotambua, kwa kufanya uzinzi, kwa kusema uwongo, kuiba, hatia yake iwayo yote, ama hata kuwaza maovu, chochote kilichokuwa katika kivuli kilicho kidogo sana, alikuwa na hatia, kwa sababu ilikuwa ni asili yake. Alikuwa mtu mwenye hatia, labda si kwa tamaa, lakini kiasili alikuwa na hatia. Naye ilimbidi atambue ya kwamba maskini huyu mwana-kondoo asiye na hatia alikufa mahali pake. Naye akamwonea huruma maskini mnyama huyo.

34 Lakini mtu huyo, mara yule mwana-kondoo hatimaye alipokufa, akiwa na damu ya huyo mwana-kondoo mikononi mwake, aliondoka humo jengoni akiwa na tamaa ile ile moyoni mwake, aliyokuwa nayo hapo mwanzo. Kwa nini? Kwa sababu uhai uliokuwa ndani ya maskini huyo mwana-kondoo . . . Uhai huwa kwenye damu. Uhai wako uko katika damu yako. Tunajua hilo. Nao ule uhai katika damu ya mwana-kondoo ulikuwa uhai wa mnyama, kwa hivyo wakati maskini chembedamu zake zilipovunjwa nao uhai ukamtoka huyo mnyama, usingeweza kumrudia mwabuduo, kwa sababu huyo mwabuduo alikuwa mwanadamu.

35 Hiyo damu ilifanyika kifuniko, lakini isingeweza kufanya upatanisho mkamilifu; kwa kuwa huyo mtu aliondoka humo jengoni akiwa na tamaa ile ile ya kutenda dhambi, kama aliyokuwa nayo mwanzoni. Lakini, akifanya hivi, alikuwa akiutazamia wakati ambapo Mwana-Kondoo mkamilifu atakuja. Naye alifanya hivyo juu ya sadaka ya kuteketezwa, kwa maana ndiyo njia pekee aliyoijua.

36 Kwa hiyo, unaona, wakati damu ilipokuwa ikimwagika, nao uhai ukamtoka huyo mnyama, haungeweza kumrudia huyo

mtu; kwa kuwa, mmoja alikuwa ni mnyama, mmoja alikuwa mwanadamu; mnyama asiye na hatia, kwa mtu mwenye hatia.

37 Lakini, loo, siku moja, yapata miaka elfu mbili iliyopita, Mwana-Kondoo wa Mungu alizaliwa katika hori ndogo huko Bethlehemu, naye akaongozwa kama kondoo apelekwaye machinjioni mwake. Yapata miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri ya leo, Yeye akafa saa tisa. Naye Mwana-Kondoo wa Mungu asiye na hatia, asiye na doa, aliangikwa kwenye msalaba wa Kalvari akafa kwa ajili ya kila mwenye dhambi. Sasa wakati mwabuduo anapokuja kwa Mwana-kondoo huyu, kwa imani! Naye huyu ni aina nyingine ya Mwana-kondoo. Si Mwana-Kondoo kama yule mwingine.

38 Hakuna mtu awezaye kuja kwa Mwana-kondoo huyu, asipovutwa na Mungu kwanza. Je, mnaona ukuu wa Mungu? Loo, natumaini hili linazama chini sana kilindini sasa. Angalieni. Mungu alijua alikuwa na kondoo katika ulimwengu huu. Alijua angekuwa na watu wa kuokolewa, nao upendo Wake ukatazama chini na kuwaona hao ambao wangeokolewa; kwa hiyo, kwa kujua tangu zamani, Yeye alilichagua Kanisa tangu zamani litakalokutana Naye huko ng'ambo, bila waa wala kunyanzi. Basi kama Mungu alihitaji Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, ilimbidi awe na kitu cha kulifanya hivyo. Hangelihitaji, haki Yake, hukumu Zake hazingemruhusu kuagiza kitu kama hicho kama kusingalikuwako na njia ya kukifanya.

39 Wala mwanadamu hawezi kufanya hivyo mwenyewe. Yeye ameshindwa kabisa. Mungu alimruhusu kuona hilo kupitia kwa sheria, kupitia kwa waamuzi, na kupitia Agano la Kale lote. Aliwatuma manabii, aliwatuma watu wenye haki, nao wakagundua ya kwamba kila mmoja alishindwa.

40 Kwa hiyo, Mungu, kwa neema Yake kuu, alituma, kutoka kwenye malango ya Utukufuni, Mwanawe wa pekee, kuchukua mahali petu.

41 Kumbukeni, kama angelisema papa wa Rumi apachukue, asingaliweza. Kama angalisema askofu mkuu wa Canterbury apachukue, asingaliweza. Kama angalimwita kasisi baba mtakatifu kuliko wote wa ulimwenguni au askofu, hangeweza kufanya hivyo. Angelikataliwa tu kadiri Yuda Iskariote alivyokataliwa. Hangeweza kufanya hivyo, kwa sababu "alizaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo," naye alihitaji upatanisho kwa nafsi yake mwenyewe.

42 Haleluya! Lakini akaja Mmoja kutoka kwenye malango ya Utukufuni; si mwingine, si mwanadamu, si mtu mwema, si Myahudi wala Mmataifa. Hakuwa chochote pungufu ya Mwenyezi Mungu, aliyefichwa katika mwili wa mwanadamu. Alikuja, Mwenyewe, kutoa Damu Yake Mwenyewe, kwa kuwa

haikuja kwa kujuana kimwili. Kujuana kimwili hakukuhusika nayo. Bali alimtia uvuli bikira, na kumzaa kutoka kwenye chembechembe ya Damu aliyoiumba, Mwenyewe, Yule asiye na hatia.

43 Ndipo wokovu wangu, wako, usiku wa leo, hautegemei ustahilifu wa matendo yetu wenyewe. Ulitegemea neema kuu ya hakika ya Mwenyezi Mungu ambaye ametuchagua katika Yeye. Hakika. Kamwe nisingeweza kuwa mkamilifu, wala wewe kamwe usingeweza kuwa mkamilifu. Wala hatudai kuwa wakamilifu. Lakini tunayo faraja hii moja, ya kwamba, imani yetu imetulia juu ya Dhabihu kamilifu ambayo tayari imepokelewa!

44 Basi tunajuaje ya kwamba tunapata Hiyo? Wakati mwabuduo anapoiweka mikono yake, kwa imani, juu ya mwili wa Bwana Yesu, na kuhisi ile hofu kuu ya dhambi, na dhihaka ya kutemewa mate usoni Mwake Mwenyewe, anapohisi kule kuugua kwa Gethsemane, yale maumivu makali ya Kalvari, na kujua ya kuwa ana hatia, na kuungama dhambi zake ipasavyo, "Ee Bwana Mbarikiwa, nina hatia. Nami sina njia nyingine ila Wewe unisaidie. Na kwa imani . . . Unaita, Roho Mtakatifu, amekuja na ananiita nije. Nami sasa, kwa imani, namkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi." Uhai ule uliotoka Kwake pale Kalvari, uitwao Roho Mtakatifu, ambao ulifichwa katika chembechembe ya Damu ya Bwana Yesu, humrudia mwabuduo na kumbatiza kwa Roho Mtakatifu, katika Mwili wa Kristo.

45 Naye amekwisha kuhukumiwa tayari. Huna haja ya kuihofia hukumu. Ninapogeuka na kuutazama maskini ule msalaba mdogo, ninatambua kuwa huo ndio . . . unauwakilisha mwili Wake. Na sasa mwili huo tayari umeshahukumiwa. Mungu hawezi kuuhukumu tena kwa haki, kwa kuwa umeshahukumiwa tayari. Mungu alipiga hukumu za mauti juu ya mwili huo. Na maadamu ninaweza kupata njia ya kujificha kwenye mwili huo, Hukumu Yake ilipigwa kwa ajili yangu na kwa ajili yako. Tuko huru! Warumi 8:1, ilisema, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Haya basi, hakuna hukumu! Sijali kijacho wala kiendacho, umefichwa chini ya Damu.

46 Tena, tunaingiaje katika Mwili huo? Wakorintho wa Kwanza 12:13 inasema kwamba, "Kwa Roho mmoja!" Roho huja vipi? Kupitia kwa Sadaka. Roho alikaa wapi? Ndani ya Damu. Kwa nini mnyama asingeweza kurudi? Alikuwa ni mnyama. Roho ya mnyama isingeweza kuja kwa roho ya mwanadamu na kuifanyia chochote, kwa sababu roho ya mwanadamu ilikuwa kiwango cha juu cha maisha kuliko mnyama. Lakini hakuna roho ya mtu mwingine ingeweza kurudi. Ikiwa una roho ya babu fulani, ni umizimu. Lakini Mungu Mwenyewe alikuja, kusudi Roho Wake Mwenyewe, ambaye ndiye kiwango cha juu kabisa cha

roho kilichoko, anaweza kurudi kwa mfano wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa mwabuduo, kupitia Damu ya Kristo, na kumwingiza katika huo Mwili. Yuko salama!

47 Tazama. Damu ya mafahali na mbuzi isingeweza kufanya kazi, kwa kuwa ilikuwa dhaifu. Sasa hebu tuanze kusoma, yapata kifungu cha 12. Vema. Damu ya mafahali na mbuzi isingeweza kufanya kazi, wala isingeweza kufanya upatanisho. Tazama.

> *Lakini huyu,* (Mtu gani? Askofu? La. Papa? La.) . . .
>
> *Lakini huyu, alipokwisha . . . kutoa kwa ajili ya* dhambi *dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;*
>
> *Tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake.*

48 Je, mko tayari? Mko tayari kwa ajili ya Neno? Sikilizeni Hili, kisha ninawatakeni mliache lizame ndani. Sikilizeni kwa makini.

> *Maana kwa toleo moja* (sio mwaka baada ya mwaka, sio uamsho baada ya uamsho, sio mkutano baada ya mkutano, sio siku baada ya siku) . . .
>
> Bali *kwa toleo moja* a-m-e-w-a-k-a-m-i-l-i-s-h-a (ati wamejikamilisha? Yeye amewakamilisha!) . . .
>
> . . . *kwa toleo moja amewakamilisha* (hayo ndiyo masharti ya Mungu) *hata milele hao wanaotakaswa.*

49 Haya basi. Hilo ndilo jibu la kifo cha Kristo. Hilo ndilo jibu la Kalvari. Yeye kabisa, kwa Damu Yake Mwenyewe, alizinunua dhambi zetu, na kuwakamilisha milele, waaminio Wake. Kwa hiyo, katika Kristo tunasimama bila hatia, tumekamilishwa Mbele za Mungu Mwenyezi. Sisi ni watu walionyimwa haki, kwa mafundisho yetu wenyewe; sote tumefundishwa kwamba tunapaswa kufika mahali fulani, tunapaswa kufanya jambo fulani. Hapana, ndugu yangu, si kitu ambacho umefanya; ni kile Mungu alichokufanyia! Sisi sasa, kama tumehesabiwa haki kwa imani, tumekamilishwa milele Mbele za Mungu.

50 Ndipo Yesu akasema, "Basi iweni wakamilifu." Basi, ilikamilishwa milele. Mungu, kupitia kifo cha Kristo, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, leo hii, alimkamilisha mwaminio, ambaye Yeye alitangulia kumwona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hata milele. Na wale aliowaita, amewahesabia haki. "Wale aliowajua tangu zamani, amewaita; wale aliowaita, amewahesabia haki; wale aliowahesabia haki, tayari amewatukuza." Amewakamilisha waaminio Wake!

51 Sasa angalieni, hebu turudi sasa kwenye kifungu cha kwanza.

. . . torati ikiwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, na si sura yenyewe ya mambo hayo, *haiwezi kamwe kwa dhabihu zile walizozitoa kila mwaka daima, haziwezi wakati wowote kumkamilisha* akaribiaye.

52 Angalieni "kamilisha," ndilo tunalozungumzia.

Kama ndivyo, je, dhabihu *hazingekoma kutolewa? kwa maana* mwabuduo *akiisha kutakaswa mara moja, wasingejiona tena kuwa na* dhambi.

53 Unamaanisha nini? Neno *kujiona* hapo, na tafsiri, sahihi, ni "shauku." Basi mtu akija, mwabuduo, kwa usahihi, mbele za Kristo, akiona mateso Yake, naye anajitolea kwa Kristo, na kusema, "Ee Bwana Mungu, hakuna kitu ndani yangu kinachoweza kufanya upatanisho, lakini nakutegemea Wewe kabisa," ndipo Roho huyo Mtakatifu anapoingia ndani ya moyo wa mwanadamu, swali lenyewe la dhambi linatatuliwa milele, kwa maana kila tamaa ya dhambi imeondolewa kwako. Kwa maana kama torati ingaliweza kufanya hivyo, dhabihu hizo hazingalikoma; lakini kwa kuwa haingeweza kufanya hivyo, ilimbidi Kristo afe, kutufanya wakamilifu.

54 Marafiki, kuna mambo mengi sana ambayo tungeweza kusema usiku wa leo, kuhusu ukamilifu. Sikuzote tunajaribu kuyang'oa macho ya mtu mwingine, kujifanya watakatifu kidogo tu kuliko wao—wao walivyo. Lakini kama tungaliiangalia tu ile picha, ni kwa neema ya Mungu tu kwamba tuko jinsi tulivyo.

55 Hapa wakati fulani uliopita, huko Ohio, nilijifunza somo kwa shida. Nilikuwa na mkutano kule Ohio, nami nilikuwa nikikaa nje ya mji. Kwa sababu ya wingi wa watu, nisingeweza kukaa mjini.

56 Tulikuwa tukila kwenye mkahawa mdogo wa Dunkard. Na maskini wahudumu wa kike wa kupendeza sana, na waliovalia vizuri, na safi kadiri walivyoweza kuwa, kama mama wa heshima kabisa, walituhudumia. Ilikuwa ni sehemu ndogo mbinguni, kula mahali hapo. Jiko lao lilikuwa safi sana. Ndipo Jumapili walifunga na kwenda kwenye kanisa lao. Nikaona njaa kidogo, nilikuwa ninaenda kuhubiri Jumapili alasiri.

57 Nami nikaenda kwenye maskini ninii . . . mkahawa wa kawaida tu wa Kimarekani, kupata chakula. Basi nilipoingia mlangoni, nilisikia nini ila mtambo wa kuchezea kamari! Naye mtu wa rika yangu alikuwa amesimama pale, ambaye labda alikuwa ni mtu aliyeoa, amemkumbatia mwanamke kwa mkono wake, akicheza kamari ya mashine. Sheria yetu yenyewe, mlinzi wa haki yetu, wa mali zetu, alikuwa amesimama pale akikiuka jambo ambalo alipaswa kulinda. Kwa sababu, ni haramu kucheza kamari Ohio, kucheza kamari ya mashine.

58 Ndipo nikageuka na kutazama nyuma wa hilo jengo, kulikuwako na kundi la wavulana matineja, na maskini santuri ya roki mtamboni, ikicheza. Msichana mdogo yapata umri wa

miaka kumi na minane, akiwa amevalia nadhifu sana chini ya anatomia yake kama mwanamke. Lakini alikuwa amesimama pale na mavazi yake mafupi upande wa mbele, na mmoja wa wavulana hao ameweka mikono yake juu ya huyo msichana, mahali haikustahili kuwa. Nao wanavuta sigara na kunywa pombe.

Ndipo nikawazia, "Ee Mungu, unawezaje kulivumilia hili?"

59 Kisha nikatazama upande wangu wa kulia, nilipomsikia mtu fulani akitoa mkoromo mkubwa. Na hapo aliketi mwanamke mzee, labda miaka sitini, au miaka sabini. Alikuwa amevaa zile nguo fupi chafu, zimefunika mapaja yake nusu, nao maskini mwili wake uliozeeka uliojaa makunyanzi ulikuwa teketeke ulivyoweza kuwa. Naye alikuwa amejipodoa hapa midomoni, na kitu kikubwa sana cha zambarau upande mwingine wa uso wake, kimepakwa rangi; amevaa maskini jozi ya viatu, makubadhi, na makucha ya zambarau miguuni mwake, yamepakwa rangi; makucha ya zambarau, yamepakwa rangi. Nazo nywele zake zilikatwa fupi sana, na zimetiwa mawimbi, na kupakwa rangi ya samawati. Nami nikamtazama.

60 Na kando ya hiyo meza waliketi wanaume wawili, wamelewa. Mmoja wao (ilikuwa msimu wa kiangazi) amevaa kabuti kubwa la kijeshi, amejizungushia kitambaa cha kijivu shingoni mwake, na masharubu yamejaa usoni mwake, akiteuka na kuendelea. Nao wakaomba radhi, mwanamume huyo alifanya hivyo, kutoka kwake, naye akaanza kutoka nje namna *hii*, akielekea msalani.

61 Nikasimama pale. Nami nikasema, "Mungu, kwa nini usikiangamize kitu hicho chote? Kwa nini usikizamishe tu chini ya ardhi?" Nikasema, "Je, mtoto wangu Sarah na Rebekah itawabidi kukulia chini ya upuuzi kama huo?" Nikasema, "Wewe, Mungu, katika utakatifu Wako mkuu, unawezaje kusimama na kutazama kitu kama hicho, pasipo kutuma tetemeko la ardhi na kukizamisha?"

62 Basi nilipokuwa nimesimama pale, nikimlaumu mwanamke huyo, kama nilivyokuwa, nilirudi nyuma ya mlango. Nilihisi Roho wa Mungu akinijia, ndipo nikaingia nyuma ya mlango.

63 Basi nikaona kama kitu kinachozunguka. Na kilipozunguka kasi, katika ono, ilikuwa ni ulimwengu ukizunguka-zunguka. Basi nilipotazama, mstari mwekundu uliuzunguka ulimwengu, kote ulimwenguni. Basi nilipoufikia ulimwengu, nilijiona, mvulana mdogo tu, nikifanya mambo nisiyopaswa kufanya; labda si *hivyo*, lakini ilikuwa ni dhambi. Na kila wakati nilipofanya lolote, niliona kile kivuli kikuu cheusi kikielekea Mbinguni. Ambapo, Mungu angeniua dakika hiyo.

64 Ndipo nikaona kati yangu na Mungu imesimama, imesimama ile Dhabihu kamilifu. Nikamwona amesimama pale amevikwa miiba kichwani Mwake, na mate yakining'inia usoni

Mwake. Na kila wakati dhambi zangu zingeanza kumwendea Mungu, Yeye angenyoosha mkono na kuzikamata, kama vile bamba kwenye gari. Alikuwa akinilinda na mauti. Na kila wakati ningefanya jambo lolote baya, Mungu angeniua. Bila shaka, utakatifu Wake unauhitaji. Sheria Yake inauhitaji. Na kila wakati ningefanya jambo lolote, ama ukifanya jambo lolote, Damu ya Yesu Kristo hutumika kama bamba. Nami nikaona ule mstari mwekundu ulimaanisha hivyo, basi, ya kwamba ile Damu ingali inaishikilia dunia.

65 Basi wakati nimesimama, nikitazama, nilimkaribia kidogo nilipomwona. Nami ningeweza kumsikia akisema, "Baba, msamehe, hajui atendalo." Nami nikatazama chini, na hapo palikuwa na kitabu. Na palikuwapo na Malaika anayerekodi pale, na amesimama kando Yake. Na kila nilipotenda dhambi, iliandikwa kwenye kitabu. Na jina langu lilikuwa juu yake. Nami nikatambua kwamba siku moja, mimi . . . huo mchirizo wa Damu ungeondolewa na ingenibidi kusimama Mbele za Mungu, pamoja na maisha yangu ya dhambi. Lakini, niliona, kwa rehema Zake alikuwa anaizuia hukumu yangu.

66 Nikamwendea, kwa unyenyekevu. Nilipiga magoti, nikasema, "Ee Yesu, Ewe Mwana wa Mungu, sistahili kuja Mbele Zako. Lakini je, utanisamehe yale niliyofanya?"

67 Akaugusa ubavu Wake kwa mkono Wake, akakitwaa kile kitabu cha kale na kuandika "amesamehewa" juu yake, akakitupa nyuma Yake, na dhambi zangu zikatoweka! Kisha akanitazama kwa ukali, usoni, akasema, "Sasa nimekusamehe, lakini unataka kumhukumu." Basi nikaona ilivyomaanisha.

68 Nilipokuwa nikitoka kwenye hilo ono, nilimwendea. Nikasema, "U hali gani?"

69 Alikuwa akinywa pombe. Alinitazama, naye akasema, "Loo, aloo."

Nikasema, "Naweza kuketi chini?"

Akasema, "Nina mwenzangu."

70 Nikasema, "Silimaanishi hivyo, mama. Ninataka tu kuzungumza nawe, kwa dakika moja."

Akasema, "Keti."

71 Nami nikasema, "Mama, dakika chache tu zilizopita, nikisimama kule nyuma ya mlango ule . . . " Nikaanza kumwambia. Basi nilipoanza kutazama, machozi yakaanza kutiririka kwenye mashavu yake. Naye akaniambia . . . Nikasema, "Mama, humaanishi kufanya mambo haya. Yesu alikufa, na hukumu za Mungu zimezuiliwa na Damu Yake. Humaanishi kufanya hivi."

72 Naye akasema, "Hapana, bwana." Akasema, "Baba yangu alikuwa shemasi kanisani. Nililelewa katika nyumba ya Kikristo. Mimi na mume wangu tulikuwa wafuasi waanzilishi,

na tuliishi maisha ya Kikristo." Akaanza kuniambia, baada ya kifo chake. . . Alikuwa na wasichana wawili wadogo, naye akapotoka. Na jinsi hao wasichana walivyokuwa wamemwacha, naye alikuwa ameyatupilia mbali maisha yake. Naye alifikiri hapakuwapo na tumaini tena kwake.

73 Lakini nikasema, "Mungu, umrehemu! 'Wale aliowajua tangu zamani, amewaita.'"

Akasema, "Kwani wewe ni Kasisi Branham, kutoka kule chini?"

Nikasema, "Ndimi."

74 Akasema, "Ninajionea aibu, kuketi hapa namna hii." Akasema, "Unafikiri kunaweza kuwako na nafasi kwa ajili yangu?"

75 Nikasema, "Yesu ameinyoosha mikono Yake, akikungojea wewe uje, mama." Ndipo hao watu wengine wakaanza kukaribia. Nami nikasema, "Je, unaweza kujongea hapa sakafuni pamoja nami?"

Akasema, "Nitafanya hivyo, bwana."

76 Nikamshika mkono. Nikasema, "Wewe ni karibu umri wa mama yangu. Je, unaweza kupiga magoti hapa pamoja nami, sakafuni?" Na hapo sakafuni, tulipasambaratisha mahali hapo alasiri hiyo, kuwa mkutano wa mtindo wa kale. Ndipo Mungu akamwokoa mwanamke huyo, kwa neema Yake. Akavaa nguo akaja mkutanoni, na, nijuavyo mimi, anaishi maisha ya Kikristo usiku wa leo.

77 Ni kitu gani? Loo, Mungu anahitaji ukamilifu! Anahitaji toba yako. Anahitaji uaminifu wako Kwake. Lakini anatazama usiku wa leo. Haijalishi umetenda dhambi kiasi gani, kidogo kiasi gani au kwa wingi kiasi gani, ungali ni mwenye dhambi, wala huwezi kuingia kwa njia nyingine ila kwa Yesu Kristo, ile Dhabihu ya Mungu inayotosheleza kwa yote. Na ndani Yake umekamilika milele. Liwazie! Sio chochote unachofanya. Sio kurasa mpya unazofungua. Sio maisha mapya unayoanza. Ni kukiri kosa lako, na neema ya Mungu kwako. Hiyo inakuleta kwenye ukamilifu, ndipo umekamilika katika Yesu Kristo.

78 Ninatumaini, usiku wa leo, rafiki yangu, wakati tukiwa hapa katika wakati huu muhimu sasa, wakati maamuzi hayana budi kufanywa baada ya kusikia hadithi hii. Huenda hujawahi kuisikia hapo awali. Lakini huwezi kutoka nje ya moja ya milango hiyo mtu yule yule uliyeingia, huna budi kutoka ukiwa bora ama mbaya zaidi.

79 Basi tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo, ninawatakeni mfikirie sana juu yake. Vipi kuhusu nafsi yako usiku wa leo? Yesu Kristo alikufa kwa ajili yako.

80 Unasema, "Ndugu Branham, ninapoweza kuacha kuvuta sigara, ninapoweza kuacha kunywa pombe, ninapoweza

kunyoosha jambo hili, nitafanya hivyo." Loo, kamwe haitafanywa vizuri. Hutaweza kamwe kufanya hivyo. Kwa nini usije tu jinsi ulivyo? Na, kwa imani, uende kwenye Kijito kile, kilichosababishwa na majeraha Yako, ndipo upendo wa ukombozi uwe ndio wimbo wako, na utakuwa mpaka utakapokufa.

81 Kwa nini kuchukua kibadala? Kwa nini kujaribu kuingia na kanisa lako? Kwa nini kujaribu kuingia kwa sababu umeacha kunywa pombe au kuacha kusema uwongo? Ingia kwa njia ya ukamilifu! "Kwa maana, kwa Dhabihu moja, amewakamilisha milele wale waliotakaswa."

"Je, ninapataje kutakaswa?"

82 Ungama dhambi zako Mbele za Damu ya Yesu; nao Uhai unaotoka katika Damu hiyo, unamrudia mwabuduo, na kumtakasa kutokana na tamaa za mambo ya ulimwengu. Kwa maana, kwa Dhabihu hiyo itoshelezayo kwa yote, Yeye ametutakasa; Roho mmoja, sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja. "Sasa hakuna hukumu ya adhabu kwao walio katika Kristo Yesu, kwa wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili, bali Roho." Ikiwa unajaribu kutembea kwa Roho, na bado una tamaa ya mwili, Dhabihu haijatumika vya kutosha kwako. Lakini mwabuduo akiisha kutakaswa, hana tena tamaa ya dhambi.

83 Hiyo ilikuwa ni Kalvari. Sio mahali pa kuuzia maua, au mahali padogo pa kufanya *hiki* au *kile*. Palikuwa ni mahali ambapo Mungu na mwanadamu walipatanishwa. Palikuwa mahali ambapo amani na usalama kamili uliletwa kwa wanadamu. Unaweza kwenda pamoja nami, usiku wa leo, rafiki yangu mwenye dhambi, Kalvari, na kwa imani upake Damu hii kwenye nafsi yako mwenyewe, na kumwacha Roho Mtakatifu aje na kukutakasa kwa Dhabihu Yake kuu?

84 Kabla hatujaomba, unaweza kuinua mkono wako kwa Mungu, na kusema, "Unirehemu, Mungu. Sasa naungama dhambi zangu zote, katika usiku huu wa Ijumaa Kuu. Nami ninayathamini mateso makuu ambayo Kristo alinifanyia. Sasa ninasalimisha mapenzi yangu mwenyewe, malengo yangu mwenyewe na kila kitu, kukufuata Wewe tangu siku hii, na kuendelea." Je, utainua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi. Huo ndio uamuzi wa moyo wangu"? Je, kuna yeyote, usiku huu mkuu, tunapongojea kwa muda kidogo tu? Huku upande wangu wa kulia, hakika kuna mmoja kando hapo. Je, unazionea aibu dhambi zako? Je, unaona aibu kwa yale uliyofanya?

85 Ulimwengu usiku wa leo unatafuta mashujaa. Nao una mashujaa, tukizungumza kimwili.

86 Siku moja huko Uswisi, wakati Waswisi wa Uswisi walipokuwa hatarini, kundi dogo la Waswisi lilikuwa

limekusanyika nje makondeni, kulinda—kulinda uchumi wao. Hilo jeshi kubwa la uvamizi lilikuwa kubwa mno kwao; wote walikuwa wamefunzwa, walikuwa na mikuki mikubwa na ngao. Hao Waswisi wasingeweza kufanya lolote ila kukata tamaa. Walizingirwa nyuma ya mlima. Ndipo akatokea shujaa. Ilibidi mtu fulani afe. Na kama wakishindwa vita . . .

87 Hawakuwa na chochote ila visu vikuukuu vya mundu, na mawe, fimbo, za kupiga nazo vita. Huku, jeshi vamizi likionekana kama ukuta wa matofali. Kama wangeshikwa mateka, maskini wake zao wapendwa wangebakwa, wasichana wao wachanga wangebakwa, watoto wao wachanga wangeuawa, vichwa vyao vingepasuliwa, nyumba zao zingetoweka, kila kitu kingepotea.

88 Basi kulikuwa na mtu, ambaye jina lake husahaulika haraka sana, aitwaye Arnold von Winkelried. Akajitokeza, akasema, "Watu wa Uswisi, leo hii natoa maisha yangu kwa ajili ya Uswisi." Akasema, "Ng'ambo tu ya mlima ule kuna nyumba ndogo nyeupe. Nina mke na watoto watatu wanaoningojea. Lakini hawataniona tena, kwa maana, leo hii nayatoa maisha yangu kwa ajili ya Uswisi."

Wakasema, "Utafanya nini, Arnold von Winkelried?"

89 Akasema, "Nifuateni, na mfanye vizuri sana mwezavyo na chochote mlicho nacho."

90 Ndipo akaliangalia lile jeshi mpaka akaona ambapo mikuki iliposhikamana sana. Basi akatupa mikono yake hewani, akakimbia kuelekea ukuta huo mkubwa wa matofali ya mikuki, na kupiga mayowe, "Simile uhuru uingie! Simile uhuru uingie!" Mikuki mia moja ikageuzwa ili kulikabili shambulizi lake; akaipanua mikono yake na kuielekeza kwenye kifua chake mwenyewe, ambayo ilimkandamiza chini, naye akafa nchani mwa mikuki hiyo. Waswisi hao wakamfuata kwa marungu na fimbo. Onyesho hilo kuu la ushujaa lililishinda jeshi hilo kabisa, mpaka hao Waswisi wakawapiga na kuwafukuza nchini. Nao hawajawahi kuwa na vita kuanzia siku hiyo, tangu.

91 Hebu simama Uswisi na utaje jina la Arnold von Winkelried, utaona machozi yakitiririka kwenye mashavu yao. Kwa nini? Aliiokoa nchi yao. Hilo lilikuwa ni tendo kuu la shujaa. Linalinganishwa kwa nadra, wala kamwe halijazidiwa, humu duniani.

92 Lakini, loo, lilikuwa jambo dogo kwa kile kilichotokea siku moja! Wakati jamii ya Adamu waliposimama, pepo wachafu wakiingia kutoka kila upande, manabii walikuwa wameshindwa, sheria ilikuwa imeshindwa, dhabihu za fahali na wana-kondoo zilikuwa zimeshindwa, asili ya mwanadamu ilikuwa imeshindwa, kila kitu. Nayo maskini jamii ya Adamu ikasimama, imeshindwa; imeshindwa kwa wingi na mashetani, ushirikina, maradhi, magonjwa. Kulikuwa na Mtu aliyetoka

Mbinguni, na kusema, “Leo hii nitakufa kwa ajili ya jamii ya Adamu.” Alikuja duniani na akafanyika mwili. Alitazama moja kwa moja chini katikati ambapo mikuki ilishikana sana. Hofu iliyo nyeusi sana ya mwanadamu ilikuwa ni kifo, Naye akayachukua mauti kifuani Mwake. Na pale Kalvari akailipia dhabihu, na kupiga mayowe, “Simile Uhuru uingie!”

93 Naye analipigia kelele Kanisa Lake, “Chukueni Hii niliyowaachia, Damu Yangu na Roho Yangu, na kupigana na kila mlicho nacho.” Tunaweza kushinda usiku wa leo, kupitia Hilo, rafiki. Unaweza kumfukuza shetani kutoka kwako. Kila adui wa kale aliye maishani mwako, anaweza kufukuzwa kwa Damu na Roho wa Kristo, nawe unaweza kusimama mkamilifu katika Uwepo Wake. Kristo alifanya njia!

94 Je, unaweza angalau kumwinulia mkono wako, na kusema, “Nisamehe”? Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine, “Unirehemu, Mungu, sasa nakiri makosa yangu”?

95 Je, kuna baadhi ya washiriki wa kanisa vuguvugu wanaoenda kanisani kila siku, na labda kujaribu kuwa watauwa wawezavyo kuwa, lakini hata hivyo unajua kwamba hasira na kutojali, na ubinafsi, tabia zinakukandamiza chini hata huna ushindi? Je, ungetaka kusafishwa kwa Damu, usiku wa leo, kutokana na hayo yote? “Kwa kuwa mwabudu akiisha kutakaswa mara moja hana dhamiri tena . . . ” Je, ungependa kuinua mkono wako, wewe mshiriki wa kanisa? Mungu akubariki, mama. Inua mikono yako na kusema, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi.” Mungu akubariki, mama. Hiyo ni sawa. Hilo ni ninii halisi . . . Hilo ni jambo la halisi kufanya. Mungu akubariki huko nyuma, bwana.

96 Mtu mwingine inua mkono wako, useme, “Unirehemu, Mungu. Najua nakiri Ukristo, lakini siuishi. Najua siuishi. Na moyoni mwangu, kwa kweli siko sawa na Wewe. Nataka kuwa mmoja wa wateule wa Mungu. Ninahisi moyoni mwangu kwamba ndivyo nilivyo mimi, lakini sijawahi kuweka kando mzigo unizingao kwa urahisi. Nami nataka kuiweka kando usiku wa leo. Na, kwa neema ya Mungu, nitafanya hivyo. Niombee.” Je, unaweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki, mama. Mtu mwingine. Kidogo tu, tunasubiri.

97 Tunapongojea kwa utulivu, kila mtu sasa huku mumeinamisha vichwa vyenu katika maombi, uvumisheni huu polepole sasa.

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotoka kwenye mishipa ya Imanueli,
> Nao wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya . . .
> Hupoteza doa lao lote la hatia,
> Hupoteza . . .

98 Je, si uliwazie tena hivi sasa? Usijaribu kuliondosha. Kristo yuko mkononi mwako.

99 Pilato aliijaribu, asubuhi ya leo, yapata saa kumi na mbili; lakini mikono yake bado imejaa damu, ina hatia na imejaa damu. Unajua kilichompata. Alienda Uswisi, miaka mingi baadaye, akarukwa na akili, akajitumbukiza katika dimbwi la maji akafa. Asubuhi ya leo, huko Uswisi, mamia ya watu wamekuja kutazama tamasha hilo, maji ya samawati huchemka kutoka chini ya shimo hilo kubwa la maji. Yanafanya hivyo kila mwaka. Ni hadithi ya zamani, wanasema kwamba Mungu aliyakataza maji kuisafisha mikono yake.

100 Ndugu, haijalishi umebatizwa mara ngapi, chochote unachojaribu kufanya, hakuna kitu kitakachoisafisha mikono yako ila Damu ya Kristo. Mungu aliyakataa. Nayo hayo maji ya samawati, baada ya miaka elfu mbili, karibu hivyo, bado yanachemka. Mungu anayakataza. Kujidai kwako hakuwezi kuzisafisha dhambi zako. Hakuna chochote ila Damu ya Yesu! Liwazie sasa. Tutaomba, kwa muda kidogo tu.

101 Sijui kama ningeweza kuuliza kitu fulani usiku wa leo. Aliposimama pale kwenye ukumbi wa hukumu wa Pilato, asubuhi ya leo, na kusema, "Kama Ufalme Wangu ulikuwa wa ulimwengu huu, ningeweza kuongea na Baba Yangu na mara moja angenitumia Mimi majeshi kumi na mawili ya Malaika." Wakati, mmoja wao angeweza kuuangamiza ulimwengu. "Ningeongea Naye, na majeshi kumi na mawili ya Malaika wangekuwa chini ya mamlaka Yangu." Angeweza kufanya hivyo. Bali alisimama pale, mpole na mnyenyekevu, kuyachukua mauti yako na kuzichukua dhambi zako.

102 Je, utashukuru vya kutosha kwa ajili ya Sadaka hiyo usiku wa leo, ninyi ambao mnaihitaji, na mnahitaji baraka za Mungu, je, mtasimama kwa miguu yenu kwa ajili ya maombi haya? Simameni tu kwa miguu yenu, ninyi mnaotaka kukumbukwa katika maombi haya, mkisema, "Mungu, unirehemu. Nina hatia, nimefanya mambo mabaya, na sasa nataka kukubali msamaha wangu kupitia Kristo Yesu." Je, utakuja kwa miguu yako kwenye wakati huu tu? Mungu akubariki, ewe msichana. Huo ni ujasiri. Endelea tu kusimama hapo.

103 Je, unataka kuniambia uliinua mkono wako, halafu huna uaminifu wa kutosha kusimama kwa miguu yako? Je, Injili imewahi kukufanyia uzuri gani? Loo, kuiga mambo namna hii, kumchezea Mungu! Saa imekaribia, moja ya siku hizi bomu la atomiki litapiga hapa mahali fulani, katika moja ya hivi viwanda vikubwa vya baruti. Hakutakuwako na hata sekunde moja ya kuliwazia. Itakuwa imechelewa sana wakati huo, na labda kabla ya Pasaka ijayo, au hata Pasaka hii. Hivi hutasimama sasa, useme, "Mungu, unirehemu mimi, mwenye dhambi. Sasa ninamkubali Kristo, kwa kujitoa Mwenyewe kama upatanisho

wa dhambi zangu. Na kwa neema Yake, na neema Yake pekee, ninakaa katika Uwepo wa Mungu." Je, utakiri kosa lako? Atakayeficha dhambi zake hatafanikiwa. Anayeungama dhambi yake, ana rehema. Ni juu yako. Anatazama.

104 Sasa, Bwana wetu Mbarikiwa, katika idadi iliyotengwa usiku wa leo wamesimama watu watatu waliotubu, mwanamume mmoja na wanawake wawili.

105 Ninapowazia, Bwana, juu ya Kalvari, wakati aliyekuwa upande mmoja, alisema, "Bwana, nikumbuke utakapokuja katika Ufalme Wako"; yule mwingine akasema, "Ikiwa Wewe ndiwe, hebu tuone muujiza, tuondoe msalabani na ujiokoe Mwenyewe." Naye huyo mwingine akasema, "Mungu, unirehemu." Ndipo kichwa Chako kikaelekea mkono wake wa kulia, na kusema, "Leo utakuwa pamoja Nami paradiso." Lakini Wewe ulimnyamazia yule mwingine, maana hapakuwapo na toba.

106 Pia, Baba Mungu, ninaomba kwamba hawa waweze... Nitaamini kwamba wao ndio watatu pekee humu jengoni, wanaohisi kwamba wanahitaji kukiri makosa yao. Lakini kwamba wamepitia njia itoshelezayo kwa yote, njia ya msalaba. Wasamehe, Bwana, na uwabariki. Wamesimama hapa usiku wa leo; kama vile ulivyowasimamia, katika ukumbi wa hukumu wa Pilato; kama ulivyowasimamia, kati ya Mbingu na nchi, jua liliposhuka na mwezi haukutoa mwanga wake, nalo pazia la hekalu likapasuka kutoka juu hadi chini. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawabariki na kuwapa rehema Zako, na kuwatakasa kwa Damu Yako. Na kuwabatiza kwa Nguvu Zako za utakaso, katika Mwili wa Mwanao Mwenyewe, Kristo Yesu, ndipo wamehifadhiwa kwa wakati na Umilele. Wabariki hao wengine wanaojisikia kuwa wako sawa, kwamba tayari wamekutana na hili na wakafanya hivyo. Ninaomba baraka hii kwao, katika Jina la Kristo. Amina.

107 Mungu awabariki. Na nyinyi mnaosimama karibu na wale waliosimama, njoni na muwape mikono, mtu fulani, na kusema, "Bwana akubariki," hiyo ni kweli, kama mkono wa ushirika.

108 Sasa tumechelewa kidogo tu katika ibada zetu. Ni wangapi wanaompenda Bwana Yesu, inua mkono wako? Nashangaa, kwa unyamavu sasa, ama kwa utulivu tu tuwezavyo, katika ukumbusho wa Yeye aliye kila mahali, aliye hapa usiku wa leo, kama tungeweza kuimba kwa upole.

> Ilikuwa pale msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia,
> Huko chini kwa ajili ya kutakaswa na dhambi nililia;
> Pale moyoni mwangu (ulipotimiza masharti, ukaweka mikono yako juu Yake), hapo

moyoni mwangu ilipakwa Damu;
Loo, utukufu kwa Jina Lake!

Hebu na tuimbe kwa upole sasa, tunapomwinamishia vichwa vyetu.

Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu,
Huko chini kwa ajili ya kutakaswa na dhambi nililia;
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!
Utukufu kwa jina Lake la thamani!
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

109 Sasa kimyakimya, huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Ninyi mliookoka, semeni:

Loo . . .

Inua mkono wako sasa.

Loo, Chemchemi ya thamani inayookoa kutoka dhambini!
Nimefurahi sana nimeingia ndani;
Hapo Yesu huniokoa na kuniweka safi;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake la thamani!
Utukufu kwa Jina Lake la thamani!
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

110 Sasa mikono yenu ikiwa chini, vichwa vyenu vimeinamishwa. Niliwaza tu; mtu alipiga simu muda mfupi uliopita, na kusema mtu fulani alitaka kukumbukwa usiku wa leo katika maombi, kwa ajili ya mwili wao. Hawangeweza kurudi kwenye mkutano wa Jumapili usiku, kwa ajili ya ibada kuu ya uponyaji. Je, mnaweza kusimama kwa miguu yenu, ninyi mnaotaka kukumbukwa katika maombi hayo sasa hivi?

. . . Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa . . .

111 Sasa huku mmeviinamisha vichwa vyenu. "Alijeruhiwa kwa makosa yako, akachubuliwa kwa maovu yako, adhabu ya amani yako ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake uliponywa."

Utukufu kwa Jina Lake!

112 Sasa, Baba Mbarikiwa, tunapokaribia msalabani kwa unyenyekevu sasa hivi, ambapo neema na rehema zilinipata, hapo Nyota Ing'aayo ya Asubuhi inaangazia miale Yake karibu nami. Hawa wagonjwa wamesimama katika Uwepo Wako. Wanaamini sasa hivi, ya kwamba kwa imani, wanautazama ule

mgongo uliovuliwa nguo, kule. "Na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Baba Mtakatifu kuliko wote, tunakuja tukiungama imani yetu, tukiamini kwamba unaiponya miili yetu iliyo migonjwa, kupitia yale mateso makuu ya Bwana Yesu. Nasi tunatoa kwa ajili ya watu hawa wanaosimama, maombi ya imani, ambayo uliahidi yangewaokoa wagonjwa. Nasi, pamoja, kama kundi la waumini Wako usiku wa leo. Ulisema, "Walipo wawili au watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao." Na tunawaombea rehema, kwamba neema Yako iguse nafsi zao za ndani sana, kwamba kitu fulani kitatia nanga kwa kilindi sana; hata watajua ya kwamba Kristo yuko hapa na amesema nao, akisema, "Mtoto Wangu, nimeupeleka ugonjwa wako pale Kalvari. Sasa nitwikeni tu fadhaa zenu zote, kwa maana Mimi hujishughulisha sana na mambo yenu." Na jalia waponywe, kwa kila chembe, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

113 Na wanapoketi sasa, mtu fulani aliye karibu nao, wawekee mikono, mtu aliyekuwa akiwaombea. Biblia ilisema, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa; watapata afya." Bwana abariki.

114 Kama sijakosea, si ninamtazama yule mtu aliyeponywa hapa siku chache zilizopita, ama Jumapili kadhaa zilizopita, ambaye alikuwa kiziwi au kitu fulani masikioni? Naona ukiufurahia mkutano usiku wa leo. Unanisikia vizuri sasa? Hilo ni zuri. Ajabu! Simama tu kwa miguu yako kwa muda kidogo. Ni wangapi wanamkumbuka akiwa hapa? Naye alipitia kwenye mstari wa maombi, akamrudisha jukwaani, naye Bwana akamponya na kumfanya mzima. Bwana atukuzwe! Asante, ndugu, kwa ushuhuda wako. Ingeweza kupitia kwa dazani kadhaa! Lakini Yeye si ni wa ajabu?

115 Sasa, tunataka kuwaona kesho usiku, mapema. Na kisha Jumapili asubuhi, mapema. Jumapili alasiri, na iwapo mnaweza kurudi kwa ibada ya uponyaji Jumapili usiku. Hata tutakapokutana, naomba tusimame na kuimba wimbo wetu wa kufumukana, "Peleka Jina La Yesu."

> Peleka Jina la Yesu,
> Mtoto wa huzuni na majonzi;
> Litaninii furaha na faraja . . .

Geuka moja kwa moja na upeane mikono sasa na kila mtu.

> Peleka kila uendako.

> Jina la thamani . . .

Geuka moja kwa moja na kupeana mikono.

> Loo, ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
> Jina la thamani, Jina la thamani, Loo ni tamu
> jinsi gani! Ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa angalia huku.

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! Loo, ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! Tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

116 Sasa kumbukeni kwaya ya Neville, matangazo ya waimbaji wanne asubuhi, WLRP, saa tatu. Na ya Ndugu Stricker inakuja saa tatu na dakika arobaini na tano, Jumapili asubuhi. Nilikuwa tu nikimtengenezea kanda alasiri ya leo, juu ya ufufuo.

117 Na sasa, hata tutakapoonana tena, baraka za Bwana ziwe pamoja nanyi, tunapoinamisha vichwa vyetu. Nami nitamwomba rafiki yangu mwema na ndugu, Ndugu Palmer, kutoka Macon, Georgia, ikiwa ataliruhusu kusanyiko hili lifumukane kwa kuomba dua, wakati tukiomba. Ndugu Palmer.

UKAMILIFU SWA57-0419
(The Perfection)
MFULULIZO WA UAMSHO WA PASAKA

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Ijumaa Kuu jioni, tarehe 19 Aprili, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org